



## KUZUIA WADUDU Toleo, TPC 8

### Mpekecha shina

*(Pink stalk borer, Sesamia calamistis)*

*Mdudu huyu ni maarufu katika sehemu nyingi za Afrika*

#### **Mahasimu**

Mdudu huyu huvamia mahindi, mtama, mawele, wimbi, mpunga, miwa na aina nyingi ya nyasi.

#### **Dalili**

Viwavi hawa huvamia shina na kupekecha huku shina likinyauka na kupunguza idadi ya mazao. Mmea huweza kukauka.

#### **Kutambua**

Kiwavi kilicho komaa ni urefu wa 30mm na upana wa 3.5mm. Kichwa ni cha rangi ya hudhurungi, mwili ni wa manjano-hudhurungi na vidota vya rangi nyekundu-nyeupe kwa mgongo.

#### **Kizazi**

Mayai hutagwa kwenye majani katika kikundi cha 40. Mayai huanguliwa baada ya wiki moja na viwavi kuvamia shina moja kwa moja. Baada ya wiki 6 hadi 10 nondo hujitokeza. Kipindi cha nondo ni kati ya siku 10.

Nondo aliyetokeza ni wa rangi ya manjano-hudhurungi na vidota vyeusi kwenye mabawa ya mbele. Nondo wa kiume (mabawa ya 22 hadi 33mm) ni mdogo kuliko yule wa kike (Mabawa ya 24 hadi 36mm). Mabawa ya nondo wa kiume ni meupe. Nondo huishi hadi siku 30 kulingana na hali ya hewa

#### **Kuzuia na Kukabili**

**Mtego wa mwangaza:** Mtego huu waweza kusaidia katika kukadiri idadi ya nondo na viwavi vya mpekecha. Mtego wa mwangaza huweza kutabiri iwapo viwavi hawa watazuka. Kiunzi kilicho tengenezwa na mwanzi huning'inizwa taa, kisha chini ya taa kuna bakuli la maji. Tahadhari yapaswa kuchukuliwa ili kuepusha visa vya moto.

**Mzunguko wa Mimea:** Mfumo huu wa kilimo hufaa sana katika kuharibu utaratibu wa kizazi cha wadudu au magonjwa. Ni muhimu basi kufanya mzunguko ili kupanda aina ya mimea isiyo shambuliwa. Wadudu wataangamia kwa kukosa mmea wa kuhisimu.

**Vibweta-kunde:** Kupanda mahindi na kunde hupunguzwa hasara itokanayo kwa mpekecha shina.

**Kutunza bustani:** Ubuu na mabaki ya mimea yaliyo shambuliwa yapaswa kuzikwa chini wakati wa kulima au hata kuchomwa iwapo sehemu ilivamiwa kupita kiasi.

**Mkojo wa Ng'ombe:** Utahitajika kukusanya mkojo. Nchini Sri Lanka, zizi la ng'ombe hutengenezwa kwa kuinuliwa sakafu ili kuelekeza mkojo kwenye tanki. Kusanya mkojo wa ng'ombe na kuweka kwenye jua kwa wiki 2. Fifisha mkojo kwa sehemu 1 ya mkojo na sehemu 2 za maji, huu ni utaratibu wa kuua viwavi (tahadhari yapaswa kuchukuliwa ili mimea isiadhiriwe na mkojo).

## **Dawa za mimea**

**Mwarobaini (*Azadirachta indica*):** Mti huu ulitokea sehemu za India, Mwarobaini umesambaa sehemu nyingi za dunia kama bara Hindi- Kusini Magharibi na Afrika *sub-sahelian*. Mbegu zaweza kupatikana kwa urahisi. Mbegu huokotwa kisha kukaushwa. Wakati unapohitaji kutayarisha dawa, utapondaponda mbegu hizo kisha kulowesha kwa siku moja. Tumia 2 hadi 50g ya unga wa mbegu kwa lita moja ya maji. Nyunyiza mchanganyiko huu kwenye mimea iliyoadhiriwa.

**Pareto (*Chrysanthemum cinerariaefolium*):** Maua ya pareto yanayo kemikali iliyo na uwezo wa kuua wadudu. Mmea wa pareto hufanya vyema katika sehemu zenye muinuko wa 1600m, na pia sehemu zisizo tumika kwa kikamilifu. Mmea huu haufanyi vyema katika sehemu zilizo na rutuba nyingi, kwani sumu hufifia.

Chuna maua wakati wa mchana. Kausha kwenye jua. Iwapo utaweka kwa muda mrefu, kausha kisha kuweka mahali pakavu na pasipo na mwangaza. Mwangaza hufufisha ukali wa sumu. Pareto huua wadudu mara moja.

**Uvugu wa pareto:** Pondaponda maua ili kufanya ungaunga. Ongeza saruji au jivu kisha kunyunyiza ungaunga huu.

**Dawa ya pareto:** Changanya 1kg hadi 1.5kg ya maua ya pareto na 3kg ya sabuni kwenye lita 100 za maji. Chuja kwa kutumia kitambaa kisha nyunyiza mara moja. Sabuni huimarisha nguvu mara nne zaidi.

**Ryania (*Ryania speciosa*):** Sehemu zinazo tumiwa ni mizizi na shina. Mmea huu huua viwavi na nondo, japo kwa muda mrefu. Hata hivyo majimaji ya mmea huu hudumu kwenye sehemu iliyonyunyiziwa kati ya siku 5 hadi 9.

**Dawa ya Ryania:** Changanya 30 hadi 40g ya uvugu wa ryania na lita 7 hadi 8 za maji. Chuja kwa kitambaa. Nyunyiza kila baada ya siku 10 hadi 14 ili kuua viwavi.

**Ni muhimu kufahamu tabia za kizazi ili kunyunyiza kabla nondo hawajataga mayai. Nyunyizia tuu wakati viwavi wanapoanza kuvamia matawi.**

# Majulisho

Tafsiri na: **Patrick Bunyali Kamoyani, September 2004. Maragoli Kenya.**  
Email [pbkamoyani@lycos.co.uk](mailto:pbkamoyani@lycos.co.uk) or [pbkamoyani@excite.com](mailto:pbkamoyani@excite.com)  
Tel **+254-(0)-721 612 607**

---

**HDRA-** Kwa huduma za kilimo hai, Ryton Organic Gardens Coventry, CV8 3LG, UK  
Simu +44 (0)24 7630 3517 Kipepesi +44 (0)24 7663 9229 Barua pepe: [ove-enquiry@hdra.org.uk](mailto:ove-enquiry@hdra.org.uk)  
Mtandao: <http://www.hdra.org.uk>

Makala haya ni mkusanyiko wa utafiti wa kisayansi na maarifa ya kilimo hai. Maelezo haya sio bayana na viwango vya kimataifa kuhusu kilimo hai. Maelezo ya ziada kuhusu mbinu za kilimo hai yaweza kupatikana kutoka kwa HDRA. Waweza kunakili makala haya kwa sababu zisizo za kifaida. Shukrani ni kwa Charlton Community Development Trust kwa mchango wa kutayarisha makala haya.

Produced by the Tropical Advisory Service, June 2000.

This update: Jan 2005